

MARKAZ IBNU UTHAIMIN

TUSWALI NAMNA GANI ILI SWALA ZETU ZITUSAIDIE?

للمصلحة الصحيحة تأثير في
سلوك العبد وأعماله الأخرى

"Swala iliyokuwa sahihi
ina athari njema katika
mwenendo wa mtu na
matendo yake men-
gine"

فالذى يصلى بحضور قلبه وخشوع
واستحضار لعظمة الله؛ هذا يخرج
بصلاة مفيدة نافعة، تنهى عن
الفحشاء والمنكر، ويحصل بها على
الفالح

"Yeyote ambaye
an aswali kwa
kuuhudhurisha moyo
wake na kwa un-
yenyekevu na kuambat-
ana na ukubwa wa Allah
moyoni mwake , basi
huyo ataondoka na swala
yenye faida na manufaa
makubwa, itamkataza
(huko aendako) dhidi ya
maovu na machafu na
atapata mafanikio (ya
akhera) kwa sababu
yake."

أما الذي يصلى صلاة صورية؛
من واد آخر؛ فهذا لا يحصل من
صلاته على طائل"

"Ama yule ambaye
anaswali swala kwa sura
ya muonekano (wa nje
tu) pasina uhudhuriija wa
moyo wala unyenyekevu,
moyo wake upo upande
fulani na mwili wake upo
upande mwininge, huyo
hatopata faida yoyote
kutokana na swala
yake."

المنشق من فتاوى الشيخ الفوزان (54.53 / 3)

(إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ الْفُحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَلَذِكْرُ اللَّهِ أَكْبَرُ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ) العنكبوت/45

Hakika swala inakataza maovu na machafu na hakika utajo wa Allah (swala)
ni mkubwa mno, na Allah anafahamu mnayoyatenda.

قال الإمام القرطبي رحمه الله تعالى:

ثم أخبر حكما منه بأن الصلاة تنهى صاحبها ومتثلها عن الفحشاء والمنكر، وذلك لما فيها من تلاوة القرآن المشتمل على الموعظة، والصلاحة تشغل كل بدن المصلي، فإذا دخل المصلي في محرابه، وخشوع، وأختير لربه، وادركت أنه واقف بين يديه، وأنه مطلع عليه وبيراه: صلحت لذلك نفسه، وتذلللت، وخارجها ارتقاء الله تعالى، وظهرت على جوارحه هيبتها، ولم يكدر بفتر من ذلك حق تظلله صلاة أخرى يرجع بها إلى أفضل حالة. فهذا معنى هذه الأخبار؛ لأن صلاة المؤمن هكذا ينبغي أن تكون.

قلت - أي القرطبي - : لا سيما وإن أشعر نفسه أن هذا ربما يكون آخر عمله، وهذا أبلغ في المقصود، وأتم في المراد، فإن الموت ليس له سن محدود، ولا زمن مخصوص، ولا مرض معلوم، وهذا مما لا خلاف فيه.

وروي عن بعض السلف أنه كان إذا قام إلى الصلاة ارتعد وأصفر لونه، فكلم في ذلك فقال: إن واقف بين يدي الله تعالى، وحق لي هذا مع ملوك الدنيا، فكيف مع ملك الملوك؟! فإنه صلاة تنهى - ولا بد - عن الفحشاء والمنكر. ومن كانت صلاته دائرة حول الإجزاء، لا خشوع فيها، ولا ذكر، ولا فضائل - كصلاته، وليتها تجزي - فتلتك ترك صاحبها من منزلته حيث كان، فإن كان على طريقة معاصر تبعده من الله تعالى: تركته الصلاة يتمادي على بعده، وعلى هذا يخرج الحديث المروي عن ابن مسعود وابن عباس والحسن والأعمش

Huwa inanipata hali hiyo
(ya kutetemeka na kuogopa)
ninaposimama mbele
ya wafalme wa duniani,
vipi nisiwe hivyo kwa
mfalme wa wafalme wote
(ALLAH) !

قولهم: (من لم تنهه
صلاته عن الفحشاء
والمنكر لم تزده من الله إلا
بعدها) "انتهى".

"الجامع لأحكام القرآن" (13/348).

Amesema Imam Alqurtubiy Allah amrehemu
kuhusiana na tafsiri ya Aya hiyo;

"Kisha Allah ameelezea hukumu kutoka kwake ya kwamba hakika swala inamkataza mwenye kuswali na kuitimiza vema, (inamkataza) dhidi ya uovo na uchafu kwa sababu ndani ya swala kuna usomaji wa Qur'an ambayo inaambatana na mawaidha mbalimbali, na swala inaushughulisha mwili wote wa anayewali. Pindi aingiapo eneo lake la kuswalia na akanyenyekia kwa Mola wake na akakumbuka kuwa yupo mbele ya Mola wake ambaye anamuona na kumchingua; nafsi yake inakuwa njema na inanyenyekia na inajawa na uchunga wa Allah na woga wa kumuogopa Allah unaokanaka katika viungo vyake. Na haitokaribia kumtoka hali hiyo (njema ya nafsi yake) isipokuwa muda wa swala nyingine unaingia na hurejea katika swala (nyingine) akiwa katika hali nzuri zaidi. Hii ndio maana ya aya hiyo , kwa sababu swala ya muumini ndivyo itakiwayo kuwa.

Hususani pindi atakapohisi nafsi mwake kwamba huenda hii ikawa ndio swala yake ya mwisho , na hali hii ndio kusudio la kileleni kabisa, na ndilo kusudio kamilifu zaidi kwa sababu kifo hakina umri maalumu na muda maalumu (ujulikanao kwa mtu) wala hakina maradhi maalumu, na hili halina utata ndani yake (linajulikana wazi kwa kila mmoja).

Na imepokelewa simulizi kutoka kwa mmoja katika wema waliotangulia kwamba yeeye alikuwa anaposimama kuswali anatetemeka na inakuwa nyekundu rangi yake aksalizwa kuhusu sababu ya hali hiyo akajibu; " Hakika mimi nimesimama mbele ya Allah Mtukufu, huwa inanipata hali hiyo ninaposimama kwa wafalme wa duniani, vipi nisiwe hivyo kwa mfalme wa wafalme wote !

Swala ya namna hii lazima itamkataza mtu dhidi ya maovu na machafu. Na yeyote ambaye swala yake ipo katika hali ya kutimiza tu wajibu, haina unyenyekevu ndani yake wala ukumbusho wowote wala ubora wowote -kama zilivyo swala zetu leo hii - na bora hata zingekuwa zinatimiza hata huo wajibu - swala kama hizi zinambakisha mwenye kuziswali katika nafasi yake ileile aliyokuwepo mwanzo, kama alikuwa katika njia ya uovo yenyekumtenga mbali na Allah, basi swali hiyo inamua cha akiweweseka huko mbali.

Kwa ajili ya (hali ya swala kama) hii husimuliwa kutoka kwa Ibnu Masoud na Ibnu Abbaas na Alhasan na Ala'mash wakisema : ((Ambaye swala yake haitomkataza maovu na machafu basi haitomzidishia kwa Allah isipokuwa umbali))"

MWISHO

وصلى الله على محمد وعلى آله وصحبه وسلم